# NI ELIMU NA ELIMU KWANZA

Kama ilivyo ada suala la Elimu ni muhimu katika jamii yoyote  ili kuleta mabadiliko katika sekta mbalimbali za maendeleo,na ni wazi kwamba Elimu ni chanzo cha maarifa, Elimu ni Ufunguo wa maisha,Elimu ni Mwanga n.k, yote hii ni katika kuhamasisha  na kuonesha umuhimu wa suala la Elimu katika jamii zetu.

Wahenga wanao usemi usemao ukiona elimu ni ghali jaribu ujinga.Dhana hii ni muhimu kueleweka katika jamii kwa kuwa kila jambo lenye mafanikio linaanza na elimu.

Mwalimu Nyerere aliwahi kusema ili nchi iendelee inahitaji mambo manne ambayo ni Elimu, Siasa safi, watu na ardhi.

Aidha, malengo endelevu ya Umoja wa mataifa yameainisha lengo la nne  ambalo ni Elimu bora kwa kutambua umuhimu wa Elimu katika kufikia maendeleo endelevu.

Serikali ya awamu ya tano katika kuhakikisha Tanzania inafikia maendeleo endelevu inapambana kuhakikisha suala  la elimu linaboreshwa katika Nyanja zote kuanzia elimu ya msingi mpaka vyuo vikuu pasipo ubaguzi wa kijinsia,kidini   na kikabila katika kufikia malengo ya mafanikio.

Halmashauri ya manispaa ya Musoma kupitia idara ya Elimu imejipanga vyema katika utoaji wa Elimu bora katika Manispaa hiyo bila kujali tofauti zilizopo miongoni mwa wanajamii hao,hasa katika Elimu ya Msingi na Sekondari kwa kugawanya idara hii katika sehemu kuu mbili ili kurahisisha ufanyaji kazi kwa weledi.

Kwa upande wa Elimu ya Msingi hadi sasa Halimashauri ina jumla ya shule za msingi 55 ambazo shule za Serikali ni 42 na za binafsi ni 13, idadi ya shule hizi za Msingi katika halmashauri ya manispaa ya musoma kwa mfululizo wa miaka 3 imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Halmashauri ya Manispaa ya musoma hadi sasa ina jumla ya wanafunzi 43,003 kati yao 38,676 ni wa shule za serikali 4,328 ni wa shule za binafsi,idadi ya ya wanafunzi katika shule za msingi za Serikali na za binafsi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Idadi ya walimu imekuwa ikiongezeka kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi Mei 2018, ambapo mwaka 2017 upungufu ulikuwa mkubwa ukilinganisha na mwaka 2016 kwa sababu ya zoezi la uhakiki wa vyeti ambapo walimu 24 walipatikana na matatizo ya vyeti.

Aidha idara ilipokea walimu 63 wa Masomo ya sanaa waliozidi kutoka idara ya elimu sekondari ambao tayari wamepangiwa vituo vya kazi.

Kutokana na muitiko mkubwa wa uandikishaji ulotokana na Sera ya Taifa ya Elimu bila malipo,Halmashauri imeamua kutumia mfumo wa ‘double session’ ili kukabiliana na upungufu wa vyumba vya madarasa katika baadhi ya shule, hata hivyo kutokana na juhudi za ujenzi wa vyumba vya madarasa shule zenye double session zimepungua kutoka 16 hadi 12 kufikia Januari 2018 kati ya shule 42 za serikali zilizopo.

Hali ya madawati hadi kufikia mwezi Mei 2018 mahitaji ya madawati katika shule za msingi ni 12,992 na yaliyopo ni 12,774 hata hivyo shughuli ya utengenezaji wa madawati mengine 306 imeshaanza ili kuondoa kabisa tatizo la upungufu wa madawati shuleni.

Vile vile miundo mbinu katika shule za msingi mpaka kufikia Februari 2018 bado ilikuwa haijitosherezi kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, na matundu ya vyoo,katika kupambana na changamoto ya miundo mbinu halmashauri inashirikiana na jamii katika ujenzi wa miundo mbinu.

Katika elimu ya msingi suala la ufaulu imefikia katika kiwango kizuri hali ambayo imekuwa ikiridhisha, huku idadi ya wavulana ikiongoza katika ufaulu.

Kutokana na jitihada ambazo idara imejiwekea halmashauri haina wanafunzi katika shule za msingi

walioacha masomo kwa tatizo la mimba kwa mfululizo wa miaka 3 kuanzia 2015 hadi 2018.

Malengo ya jumla katika sekta hii ya elimu ya msingi ni pamoja na suala la mtambuko katika elimu kwa kupunguza maambukizi ya UKIMWI kwa wafanya kazi wa elimu ya msingi, pia kuongeza idadi ya shule zinazotumia Elimu Kwa Tehama katika ufundishaji na ujifunzaji mpaka sasa zipo 10.

Upatikanaji wa elimu wa kwa kuongeza ufaulu katika mtihani wa darasa la saba kutoka 74.56% mwaka 2017 hadi 85% mwaka 2018, kuongeza ufaulu katika mtihani wa darasa la 4 kutoka 94% hadi 100% mwaka 2018, pia kuandikisha wanafunzi wote wenye umri wa kwenda shule

Idara ya elimu msingi imeweza kufanikiwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaofaulu mtihanii wa darasa la 7 na kujiunga kidato cha kwanza,kupanda kwa uandikishwaji wa darasa la awali na kwanza, walimu kupata mafunzo ya KKK kupitia mradi wa 'EQUIP -T',hivyo kupunguza tatizo la kutokujua kusoma nkuandika na kuhesabu kwa madarasa ya kwanza hadi la nne, pia kuimarisha ukamilishwaji wa nyuma nne za walimu.

Kwa upande wa Elimu ya Sekondari Halimashauri inaenda sambamba na mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari ikiwa na lengo la kuongeza idadi ya vijana wa

kitanzania wanaomaliza elimu ya sekondari wakiwa na kiwango bora cha uelewa kinachokubalika katika jamii.

Hivyo kutokana na umuhimu wa Elimu Manispaa ya Musoma ina jumla ya shule za Sekondari 27 huku 18 zikimilikiwa na serikali na shule 7 zikiwa ni za watu binafsi, huku idadi ya walimu ikiwa na upungufu mkubwa hasa katika masomo ya sayansi pamoja na kuwepo kwa uoungufu wa miundo mbinu hasa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, nyumba za walimu, maktaba,madawati,maabara na mabweni kwa ajili ya wanafunzi wanaoishi mbaili na sule.

Katika utoaji wa elimu hii ipo changamoto kubwa inayowakabili watoto wa kike ambayo ni tatizo la wanafunzi kupata mimba inayowapelekea kusitisha masomo yao.

changamoto nyingne ni baadhi ya wanafunzi au walezi kushindwa kutoa ushirikiano kwa uongozi wa shule,viongozi wa kata na jeshi la polisi ili kuwachukulia hatua waliohusika kuwapa mimba wanafunzi.

Hata hivyo matokeo ya mtihani wa Taifa kwa miaka 3 yamekuwa yakibadilika mwaka hadi mwaka, kwa mwaka 2016 ufaulu wa mitihani kidato cha iv na cha ii kdato cha nne ilikua 60, 2017 kidato cha iv ilikuwa ni 68%.

Pamoja na mafanikio hayo idara inakumbana na Changamoto mbalimbali ikiwemo ni upungufu wa walimu 117 wa masomo ya sayansi na hisabati, upungufu wa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maabara 46 na vyumba vya madarasa 86 katika shule za sekondari , muitikio mdogo wa jamii klatika kuchangia maendeleo ya shule za sekondari na pia ufinyu wa bajeti isiyotosheleza mahitaji ya ujenzi wa miundo mbinu ya ujenzi wa shule za sekondari pamoja na uendeshwaji wa shughuli za elimu ya sekondari.

Katika kupunguza tatizo la uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi na hisabati wazazi wamehamasishwa kuomba kibali cha kuchangia fedha kidogo kwa ajili ya kuwalipa posho walimu kwa muda wa masomo ya sayansi, manispaa ya Musoma imepanga kutumia shilingi 90,000,000.00 kutoka kwenye mapato ya ndani na shilingi 207,115,800.00 kutoka serikali kuu kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa, maabara na utengenezaji wa madawati.

Pia katika kupunguza tatizo la watoto wa kike kupata mimba halmashauri ya manispaa ya Musoma imeanzisha hosteli ya wasichana katika shule ya sekondari ya Morembe,pia inashirikiana na wadau wa Elimu kupitia mradi wa WAACHE WASOME katika shule 7 za sekondari

za Makoko, Mwisenge, Buhare, Nyasho, Nyabisare, Nyamitwibiri na Iringo sekondari.

Pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali katika kuendeleza elimu jitihada za makusudi kutoka kwa wadau mbalimbali zinahitajika kuiweka elimu katika viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa ili kujiweka katika nafasi nzuri ya ushindani wa soko la ajira.